

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO
SHULE YA SEKONDARI MVOMERO, P.O BOX 2163**



Kumb Na _____

Jina la mwanafunzi _____

S.L.P _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MVOMERO, WILAYA YA MVOMERO, MKOA WA MOROGORO, MWAKA 2021.

1.0. UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Mvomero ipo Halmashauri ya Mvomero, ipo umbali wa km 2 mashariki mwa barabara kuu ya Turiani. Usafiri wa basi kutoka mjini Morogoro unapatikana katika kituo cha mabasi cha MSAMVU, nauli ni Tshs. 4,000/=. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021 (ndani ya siku saba).

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. Sare za shule

(A) SARE ZA SHULE HII KWA WASICHANA NI:

- (i) Sketi mbili (2) za kaki (American kaki) ziwe ndefu zisizo bana.
- (ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi.
- (iii) Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba visiwe na visigino virefu.
- (iv) Soksi nyeupe.
- (v) Tai inayofanana na sketi (tai fupi).
- (vi) Rangi ya hijabu ifanane na sare za shule.
- (vii) Sketi ndefu au suruali isiyo bana rangi ya American kaki (modo hairuhusiwi).

(B) SARE YA SHULE HII KWA WAVULANA NI:

- (i) Suruali mbili (2) za kaki (American kaki) zisizo bana (modo hairuhusiwi)
- (ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi
- (iii) Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba visivyo na visigino virefu
- (iv) Soksi nyeusi
- (v) Tai inayofanana na suruali (tai fupi)

(C) SARE YA MICHEZO KWA SHULE HII NI T- SHIRT YA KIJANI KWA WAVULANA NA WASICHANA.

2.2. Mahitaji ya taaluma


- (i) Daftari kumi (10)
- (ii) Kalamu
- (iii) Mkebe wa hesabu

3.0. Sheria na kanuni muhimu za shule hii ni:

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu chini ya ofisi ya Rais yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara tu baada ya kuripoti shuleni.

- (a) Heshima kwa walimu, viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na janiii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- (c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
- (d) Kushiriki katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- (g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kwa mujibu wa taratibu za shule.
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- (i) Kutunza mali za umma.


MSAFIRI H. SHAURI
MKUU WA SHULE

**MKUU WA SHULE
MVOMERO SEKONDARI
S. L. F. 2163
MOROGORO**